

## Maswali na Majibu

1. Baada ya Sulemani nani alikuwa mfalme? *Rehoboamu*
2. Watu walitaka Rehoboamu afanye nini?  
*Apunguze kodi waliokuwa wakilipa.*
3. Rehoboamu aliwapa watu jibu gani? *Aliwafanya walipe zaidi ya ile.*
4. Nini ilifanyika wakati Rehoboamu alisema walipe zaidi?  
*Kabila kumi walimkataa na kumtawaza Yeroboamu kuwa mfalme wao.*
5. Ahadi ya Mungu kwa Daudi ilitimizwa namna gani kwamba kila mara mwanawe atakuwa mfalme?  
*Mwana wa Sulemani Rehoboamu alitawala makabila 2.*
6. Ufalme wa Yeroboamu uliitwa nani? Mji mkuu uliitwa nani?  
*Ufalme wa Israeli. Mji mkuu ulikuwa Samaria*
7. Ufalme wa Rehoboamu uliitwa nani? Mji mkuu uliitwa nani?  
*Ufalme wa Yuda. Mji mkuu uliitwa Yerusalemu.*
8. Mbona Yeroboamu alitengeneza ndama mbili za dhahabu kama miungu?  
*Hakutaka waende Yerusalemu kwa sababu wangebaki Yuda na Rehoboamu.*
9. Ufalme gani ulikuwa na wafalme wote waovu? Ufalme gani ulikuwa na wafalme wengine waovu na wengine wazuri.  
*Israeli ilikuwa na wafalme wote waovu. Ufalme wa Yuda ulikuwa na wazuri na wengine waovu.*
10. Mungu alituma nani ambie watu wabadilike na wamrudie?  
*Mungu alituma manabii.*

## Mistari ya kukariri

1 Wafalme 12:14      Yeremia 25:4      Mithali 13:20

## Mazungumzo

Vile tumejifunza kwa hili somo, nini inasababisha uzuri au ubaya? Tunaweza kusababisha uzuri namna gani? Tunaweza kuheba kuingizwa kwa ubaya na watu wengine namna gani?

## Kuandika

Soma 1 Wafalme 11:28 – 36. Eleza vile nabii Ahiya alionyesha Yeroboamu kwamba atakuwa mfalme.

# Masomo ya watoto wakubwa wa CBM



## Somo la 25 Ufalme umegawanywa


**SOMA 1 Wafalme 12:1 – 30**

### SOMO

Sulemani alijenga majengo mengi ya ajabu wakati wa utawala wake. Alikuwa na watu wengi wa kufanya kazi. Watu wa Israeli walilipa pesa nyingi kama kodi kwa Sulemani. Sulemani alipokufa, mwanawe, Rehoboamu alikuwa mfalme. Watu wote walikuja Shekemu kumtawaza kama mfalme. Watu walitaka Rehoboamu awapunguzie kodi yenye baba yake Sulemani aliweka. Kodi hiyo ilikuwa juu na kufanya maisha kuwa magumu kwao.

Watu wa hekima waliosaidia Sulemani kutawala waliambia Rehoboamu kupukuza kodi. Akiwa mzuri kwa watu, watampenda na kumheshimu na kumtumikia vizuri. Rehoboamu hakutaka kupukuza kodi. Alitaka pesa nyingi kama Sulemani baba yake. Rehoboamu aliuliza vijana wenzake wamshauri. Walimshauri kwamba, watu wanatakiwa walipe kodi maradufu. Rehoboamu aliamua kusikia maneno ya vijana wenzake.

Rehoboamu aliambia watu, “Mimi nina nguvu kuliko baba yangu, Sulemani. Kidole changu kidogo ni kubwa kuliko kiuno cha baba yangu. Mtalipa kodi ya juu kuliko mliyolipa kwa baba yangu. Baba yangu alimwadhibu kwa kiboko lakini mimi nitamwadhibu kwa mijeledi.”



Watu waliudhika sana na Rehoboamu alipowambia kwamba watalipa kodi maradufu. Makabila kumi walikataa Rehoboamu. Walimfanya mtu aliyetwa Yeroboamu kuwa mfalme wao. Hawa makabila kumi walikaa upande wa kaskazini. Waliitwa taifa la Israeli. Yeroboamu alifanya Samaria kuwa mji wake mkuu. Alitawala makabila kumi za Israeli.

Rehoboamu aliachwa na kabila mbili za kutawala. Kabila ya Yuda na kabila ya Benyamini ndizo zilibaki kusini ya nchi. Hizi kabila mbili ndizo zilibaki na Rehoboamu. Ziliitwa taifa la Yuda. Mji mkuu wa Rehoboamu ulikuwa Yerusalemu. Mungu alikuwa ameahidi Daudi kwamba mzao wake atakuwa akitawala watu wake. Mungu alitimiza hii ahadi kwa kuachia Rehoboamu, mjukuu wa Daudi kabila mbili.

## YUDA

Mfalme Rehoboamu  
Kabila mbili  
Mji mkuu – Yerusalemu  
Wafalme – wazao wa Daudi  
Ibada – Mungu Hekaluni  
Wafalme wazuri na wabaya

Kutokea pale, hizi falme zilibaki zimegawanyika. Ufalme wa Yuda na ufalme wa Israeli waliendelea kugawanyika. Mungu alitimiza ahadi kwa Daudi kupitia kwa ufalme mdogo wa Yuda. Daudi alitoka kwa kabila ya Yuda. Wafalme wa Yuda walitoka kwa uzao wa Daudi.


Wafalme wa Yuda walitawala kutoka kwa mji mkuu wenye Daudi alichagua – Yerusalemu. Watu wa Yuda waliabudu Mungu kwa Hekalu yenye Sulemani alijenga. Wafalme wengine wa Yuda walikuwa wazuri; walifundisha watu kuabudu Mungu. Wafalme wengine hawakutaka Mungu. Lakini mzao mmoja wa Daudi alitawala juu Yuda vile Mungu aliahidi. Yesu atatawala milele kwa kiti cha enzi cha Daudi atakaporudi hapa duniani.

## ISRAELI

Mfalme Yeroboamu  
Kabila kumi  
Mji mkuu – Samaria  
Wafalme – wafalme tofauti tofauti  
Ibada – ndama za dhahabu + miungu  
Wote waovu


Sulemani alikuwa amejenga hekalu nzuri Yerusalemu ili watu watumie kuabudu Mungu. Watu walisafiri mara tatu kwa mwaka kwenda huko kuabudu Mungu. Yeroboamu hakutaka watu wake wasafiri hadi Yerusalemu. Aliogopa kwamba wanaweza kwenda na wabaki Yuda na watumikie Rehoboamu. Yeroboamu alitaka hizo kabila kumi zibaki Kaskazini.

Yeroboamu alifanya ndama mbili za dhahabu. Aliambia watu lazima waabudu zile miungu. Aliweka sanamu ya ndama mmoja kusini mwa nchi kule Betheli na sanamu ya ndama nyingine akaweka kaskazini kule Dani. Yeroboamu aliambia watu wake kwamba Yerusalemu ilikuwa mbali kwenda kuabudu. Mbadala lazima waabudu ndama ya dhahabu. Yeroboamu aliwambia watu wake kwamba hiyo ndama ndio mungu. Aliwafanya watu kuabudu ndama ya dhahabu.



Watu wachache waliokuwa upande wa kaskazini walitaka kuabudu Mungu kwa hivyo walienda kuishi kwa ufalme wa Yuda. Walienda Yerusalemu

Wafalme wote wa Israeli walikuwa waovu. Watu wote wa Israeli waligeuka wasimwabudu Mungu. Wafalme wa Israeli hawakuwa wa uzao wa Daudi. Kulikuwa na wafalme tofauti tofauti. Wengi wao walikuwa kama Yeroboamu, na wakafanya Israeli iwe ya dhambi. Baadaye Samaria ilikuwa mji mkuu wa Israeli.



Falme za Israeli na Yuda zilibaki zimegawanyika. Hizi falme zilikuwa hivyo kwa miaka mingi. Zilikaa kama maadui na zilikuwa zikipigana. Ufalme wa Yuda ulikuwa wakati mwingine na wafalme wazuri na wengine wabaya. Wakati kulikuwa na mfalme mzuri alifundisha watu amri za Mungu na waliabudu katika hekalu kule Yerusalemu. Lakini wafalme wabaya walifanya watu waabudu miungu. Wafalme wa Israeli wote walikuwa waovu. Waligeuza watu wa Israeli waache Mungu na waabudu miungu.

Mungu alipoleta Waisraeli kwa nchi ya ahadi, alifanya agano nao. Watu waliahidi kumpenda na kutii amri zake. Mungu aliahidi kuwabariki na kuwapa amani kwa hiyo nchi, kama watamtii. Lakini Mungu aliwambia,

kama hawatamtii na waabudu sanamu, atawaletea mataifa mengine wawapige na kuwachukua mateka.

Watu wa Yuda na Israeli waliendelea kuasi Mungu na kuabudu miungu wengine. Nabii ni mtu aliyeleta ujumbe kutoka kwa Mungu. Kuna wakati alikuwa na ujumbe wa mfalme. Wakati mwingine ulizungumza na watu. Mungu alituma manabii wengi sana kwa watu wa Israeli na Yuda. Manabii waliwambia kwamba lazima wamrudie Mungu. Manabii waliwahadharisha kwamba wakiendelea kuabudu sanamu badala ya Mungu, watafurushwa kutoka kwa nchi yao. Maadui wataleta majeshi kuwapiga. Watapelekwa mateka kwa nchi zingine.